JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI**

*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

# TANGAZO LA UBORESHAJI DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA AWAMU YA PILI NA UWEKAJI WAZI DAFTARI LA AWALI

Afisa Mwandikishaji wa Jimbo la Babati Vijijini anawatangazia Wananchi wote kujitokeza kwenye zoezi la uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga kura awamu ya pili kwa ajili ya uchaguzi mkuu, litakalo anza tarehe 16/05/ hadi tarehe 22/05/2025 na litaenda sambamba na uwekaji wazi wa Daftari la Awali

Vituo vya kuboresha daftari vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 12:00 Jioni na uboreshaji huu utafanyika ngazi ya Kata Wahusika wa uboreshaji daftari ni kama ifuatavyo:-

1. **Anaye jiandikisha kwa mara ya kwanza**:-
   - Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18
   - Raia wa Tanzania Mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambaye hakuwahi kujiandikisha kwenye daftari
   - Raia wa Tanzania atakaye fikisha miaka 18 tarehe ya uchaguzi mkuu mwaka 2025,
2. **Anaye boresha Taarifa zake**:-
   - Aliye jiandikisha awali na amehama eneo moja la uchaguzi kwenda lingine
   - Ambaye taarifa zake zilikosewa wakati wa kujiandikisha
   - Aliyepoteza au kadi yake kuharibika
   - Aliyepoteza sifa kuwemo katika Daftari la kudumu la Wapiga kura mfano aliyefariki

Aidha daftari la Awali la wapiga kura limebandikwa kwenye kila kituo kilichotumika kuandikisha wapiga kura mwaka jana.

Wananchi wote mnatangaziwa kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya uboreshaji vilivyopo ngazi ya kata na kwenda kukagua daftari la awali kwenye vituo mlivyojiandikisha mwaka jana.

***"Kujiandikisha kuwa Mpiga kura ni msingi wa uchaguzi Bora"***

David J

**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikalini**

CamScanner